23. THE PICTURE OF DORIAN GRAY

23. THE PICTURE OF DORIAN GRAY

THE PICTURE OF DORIAN GRAY ni riwaya iliyoandikwa na OSCAR WILDE inayohusu picha ya kuchora ya Dorian Gray ambayo inabeba madhambi yake kwa muda mrefu kwa kuwa aliomba hivyo. Lakini mwisho anashindwa kuendelea na maisha aliyokuwa nayo, anaiharibu picha na kukatisha uhai wake.

👉1
Mchoraji Basil Hallward yuko kwenye studio yake na rafiki yake anayeitwa Lord Henry Wotton.
Basil ni moja wa wachoraji maarufu na ambaye amekuwa haeleweki, mara kwa mara huwa anapotea na hakuna anayejua aliko. Usiri wake umekuwa unampa umaarufu mkubwa.
Lord Henry anaona picha nzuri ambayo Basil anaichora, anamwambia hiyo ni moja ya kazi zake bora kabisa amewahi kufanya. Anamshawishi aipeleke kwenye maonesho ya picha ya Grosvenor.
Basil anamjibu hataweza kufanya hivyo, kamwe hatapeleka picha hiyo kwenye maoneshi.
Lord Henry anamshangaa na kumuuliza kwa nini asipeleke picha hiyo ambayo itampa umaarufu mkubwa?
Basil anamjibu ni kwa sababu ameweka nafsi yake kwenye mchoro huo kuliko mchoro wowote ambao amewahi kuchora, hivyo kama atapeleka kwenye maonesho ni kama atakuwa ameiweka wazi nafsi yake kwa kila mtu, wakati yeye anapenda usiri.
Lord Henry anamcheka, anamwambia aache kujidanganya, hawezi kuwa na uzuri kama ulio kwenye picha hiyo. Anamwambia watu wote wanaofanya kazi za kutumia akili na kufikiria sana huwa hawawi na uzuri.
Basil anamwambia ni kweli hana uzuri wa mtu aliye kwenye picha hiyo, ila alipokutana na mtu huyo, kuna kitu cha tofauti kilikuja ndani yake, alijikuta anamkubali haraka na kutaka sana awe rafiki yake. Ni mtu pekee ambaye amemkubali kwa kiasi kikubwa na kujiona nafsi yake kupitia yeye.
Lord Henry anamuuliza jina la aliye kwenye picha, anamjibu ni Dorian Gray, walikutana kwenye moja ya sherehe na kujuana hapo na wamekuwa marafiki.
Lord Henry anamuuliza amekuwa anakutana naye mara ngapi, Basil anajibu kila siku.
Lord Henry anaiangalia picha na kutamani sana akutane na Dorian pia.
Wanatoka nje ya studio na kukaa kwenye bustani. Lord Henry anamwambia Basil amekumbuka alishasikia jina la Dorian likitajwa na shangazi yake, akimsifia ni kijana mzuri.
Lord Henry anamtaka Basil amkutanishe na Dorian, Basil anajibu hataki hilo litokee, maana anamjua atakuwa na ushawishi mbaya kwake.
Wakiwa pale kwenye bustani, mfanyakazi wa Basil anamwambia Dorian amefika yupo studio, anamsubiri.
Lord Henry anamuomba sana Basil amkutanishe na Dorian, Basil anakubali, lakini anampa sharti moja, asitumie ushawishi wake kumbadili Dorian, maana amempenda jinsi alivyo na amekuwa kichocheo kipya kwenye kazi zake za sanaa.

👉2
Wanaingia studio na kumkuta Dorian amekaa, Lord Henry anavutiwa naye mara moja, wanasalimiana na Basil anawatambulisha.
Basil anamkumbusha Lord Henry asiwe na ushawishi mbaya kwa Dorian. Lord Henry anamjibu hakuna ushawishi mzuri, ushawishi wowote ni mbaya, maana mtu anaposhawishiwa, anaacha kuwa yeye na kutaka kuwa kama aliyemshawishi.
Anaeleza lengo kuu la maisha ni mtu kuwa yeye na kukazana kuwa bora kwa namna yake na siyo kutaka kuwa kama wengine.
Amamsifia Dorian kwa ujana wake na utanashati wake, anamweleza jinsi maisha yalivyo yake.
Basil anamtaka Lord Henry atoke na kuwaacha ili afanye kazi. Dorian anasema kama Lord Henry

anaondoka basi na yeye ataondoka, maana yeye Basil huwa hamsemeshi kama anavyofanya Lord Henry.
Basil anakubali na kusema anapofanya kazi, huwa anaweka umakini wake wote kwenye kile anachofanya ndiyo maana huwa hamsemeshi. Anakubali Lord Henry abaki, Dorian anakaa kwenye jukwaa na Basil anaendelea kumchora, huku Lord Henry akiendelea kuongea.
Lord Henry anaeleza jinsi ambavyo watu hawana ujasiri wa kuyaishi maisha yao, wanawalisha na kuwavalisha wenye uhitaji huku mioyo yao ikiwa na njaa na ikiwa uchi.
Anamsifia Dorian kwamba kwa uzuri wake, dunia nzima ni yake.
Dorian anakuwa na utulivu mkubwa wakati wote ambao Basil anachora, ghafla anamwambia Basil amechoka na anataka kutoka nje apate hewa zaidi.
Dorian anatoka na Lord Henry wanaenda kwenye bustani ambapo Lord Henry anaendelea kumweleza jinsi ambavyo ujana ni kipindi kifupi.
Anamwambia uzuri alionao sasa hautadumu hivyo, miaka michache ijayo utakuwa umeondoka, hivyo anapaswa kuutumia kwa wakati huu alionao, kwa kuchagua kuyaishi maisha yake na siyo kufungwa na matakwa ya wengine.
Anamwambia lengo la maisha ni kuwa na raha na hivyo atumie ujana wake kula raha badala ya kuupoteza kwa kufungwa na maadili ya wengine.
Wanaongea kwa muda, Dorian anajiona kuna kitu kikubwa kimebadilika ndani yake, amejiona kwa namna ambayo hajawahi kujiona maisha yake yote.
Basil anawaita ndani ili amalizie kuchora, wakati wanarudi Dorian anamwambia Lord Henry ameshukuru sana kukutana naye na anaamini atakuwa rafiki mzuri kwake. Dorian anakaa kwenye jukwaa na Basil anaendelea kuchora, kunakuwa na ukimya mkubwa.
Baada ya muda Basil anawaambia mchoro umekamilika. Lord Henry anauangalia, anamwambia Basil hii ni kazi bora kabisa za michoro ambazo amewahi kuona.
Dorian anaangalia mchoro wake na kukaa kimya kwa muda, kisha anaanza kulia. Basil anamuuliza kama hajaupenda. Dorian anajibu ameupenda mno mchoro huo, analia kwa sababu anauonea wivu, anajua mchoro huo hautazeeka, ila yeye atazeeka. Hicho ndiyo kinamfanya alie, maana wakati thamani yake inashuka, ya mchoro inakuwa inapanda.
Lord Henry anasema yuko tayari kulipa kiasi chochote cha fedha ili kumiliki mchoro huo, Basil anasema mchoro huo ni mali ya Dorian.
Dorian anasema ni bora ajiue kuliko kuuangalia mchoro huo, maana unamfanya ajione hana thamani.
Basil anashangazwa na hilo, anasema mchoro huo unaweza kuharibu urafiki wao watatu, hivyo anachukua kisu ili auharibu. Dorian anamsihi asiuharibu, itakuwa ni kama amemuua yeye.
Anamwambia atauchukua mchoro huo na kuutunza vizuri.
Basil anamwambia Lord Henry kwamba Dorian amebadilika sana tangu amekutana naye, anamjibu kabla hajakutana naye alikuwa hajajijua vizuri ila sasa ndiyo amejijua.
Lord Henry anawaambia waende kwenye sinema jioni hiyo, Basil anasema hawezi kwenda maana ana kazi nyingi. Anamsihi Dorian pia asiende, ila anasisitiza ataenda.
Wanaagana, huku Basi akimkumbusha Lord Henry asisahau alichomwambia kuhusu ushawishi wake kwa Dorian.

👉3
Lord Henry anamtembelea mjomba wake anayeitwa Lord Fermor na kumuuliza kama anataarifa zozote kuhusu Dorian. Lord Henry anaanza kwa kumwambia kwamba Dorian ni mjukuu wa Lord Kelso ambaye mama yake alikuwa ni Lady Margaret Devereux.
Lord Fermor anamjibu anamkumbuka vizuri sana Lady Margaret ambaye alikuwa msichana mrembo enzi za ujana wao. Msichana aliyechumbiwa na vijana kutoka familia tajiri. Lakini cha kushangaza, akaamua kuolewa na kijana ambaye hakuwa anajulikana wala hakuwa na fedha.
Hilo halikumfurahisha baba yake ambaye aliweka mpango wa mume huyo wa mtoto wake kuuawa.
Anauawa na Lady Margaret anarudishwa nyumbani kwa baba yake lakini mahusiano yao hayawi mazuri.

Mwaka mmoja baadaye Lady Margaret anakufa na kuacha mtoto mdogo ambaye ndiye Dorian Gray.
Lord Fermor anauliza kama bado mtoto huyo yupo na kama ana mwonekano mzuri kama wa mama yake. Lord Henry anajibu ni kijana sasa na ana mwonekano mzuri sana.
Lord Fermor anamwambia anatajaria atalelewa vizuri hasa ukizingatia vifo vya wazazi wake.
Lord Henry anashukuru kwa taarifa hizo na kuaga kwa sababu anataka kuwahi chakula cha jioni kwa shangazi yake anayeitwa Lady Agatha, ambapo Dorian pia atakuwepo.
Anaenda huku njiani akifikiria jinsi historia fupi ya maisha ya Dorian aliyoipata inamfanya awe mtu sahihi kwake. Anaona Dorian yuko wazi kutumiwa na yeyote kufanywa vyovyote vile, iwe mtu mkuu au mtu wa hovyo.
Anajiambia atamshawishi Dorian aweze kuwa na maisha ya tofauti na ya wengine.
Anafika kwenye chakula cha jioni na kukuta shangazi yake akiwa na wageni wengine wa heshima ma Dorian pia akiwepo.
Anajiunga nao, wanajadili mambo mbalimbali, kubwa likiwa ni mwenendo wa vijana wengi wa Uingereza kuona mabinti wa Marekani. Wengi wanaonekana hawafurahishwi na hilo, ila Lord Henry anatetea kwamba mabinti hao wa Marekani ni warembo na wako huru kuyaishi maisha yao.
Mmoja wa wageni kwenye chakula hicho ambaye ni mwanamke mtu mzima anasema angetamani sana kurudi kwenye ujana na aishi kwa uhuru zaidi.
Lord Henry anamwambia hilo ni rahisi, akumbuke makosa yote aliyowahi kufanya akiwa kijana na ayarudie kuyafanya sasa.
Mwanamke huyo anasema atajaribu hilo. Wengine wanamtahadharisha ni hatari na mzee mmoja anaongea na Lord Henry kwa pembeni na kumuuliza kama anamaanisha kweli hayo anayosema au anatania tu. Lord Henry anamwambia ndiyo falsafa ya maisha yake.
Mkutano huo kwa ajili ya chakula unaisha na watu wanatawanyika, baadhi wanamwalika Lord Henry wawe na mkutano naye ili kuichimba zaidi falsafa yake. Lord anawaambia yuko tayari wakati wowote wanaotaka mkutano huo.
Dorian anamfuata Lord Henry na kuwambia anataka waondoke wote, Lord Henry anamwuliza si alikubaliana na Basil kwakna ataenda kwake? Dorian anajibu anachotaka kwa sasa ni kuwa na yeye Lord Henry tu na kumsikiliza akiwa anaongea.
Lord Henry anamwambia kwa sasa ameshaongea ya kutosha, anaenda kuangalia maisha kama na yeye anataka kuangalia naye maisha anakaribishwa.

👉4
Mwezi mmoja baadaye Dorian ameenda nyumbani kwa Lord Henry ambaye walipanga kukutana, ila hamkuti, inabidi amsubiri. Lord Henry huwa ana tabia ya kuchelewa kwenye kila jambo, msingi wake ukiwa kwamba kuwahi ni kupoteza muda.
Akiwa anamsubiri Lord Henry, mke wake anakuja na kujitambulisha kwake, anamwambia japo hawajawahi kuonana amekuwa akimsikia Lord Henry akimsifia mara kwa mara.
Wanajadiliana kuhusu muziki na mke wa Lord Henry anamwambia Dorian kwamba maoni yake ni kama ya Lord Henry kitu ambacho amekuwa anakiona kwa marafiki wake wote. Kwamba kila rafiki wa Lord Henry huwa anaishia kuwa na maoni kama yake.
Wakiwa hapo Lord Henry anafika na kuomba samahani kwa kuchelewa. Mke wake anawaaga na kuwaambia kuna mahali anawahi.
Baada ya mke wake kuondoka, Lord Henry anamwambia Dorian kamwe asioe kwenye maisha yake. Anasema wanaume huo kwa sababu wamechoka na wanawake huolewa kwa sababu ya udadisi, ila mwisho wa siku wote huishia kukatishwa tamaa.
Dorian anamjibu hadhani kama ataoa kwa sababu kwa sasa yuko kwenye penzi zito na muigizaji anayeitwa Sibyl Vane.
Lord Henry anashangazwa na hilo na kumtaka amweleze zaidi kuhusu mwanamke huyo.
Dorian anamweleza alimjulia kwenye nyumba ya sinema ambapo binti huyo alikuwa anaigiza mchezo wa Romeo and Juliet wa Shakespeare.
Anaeleza ni binti mrembo na mwenye akili sana, amevutiwa naye sana na kwa sasa huyo ndiyo kila

kitu kwake.
Lord Henry anamtaka awe makini, hilo ni penzi lake la kwanza hivyo asifunge milango yake. Kwani haijalishi mwanamke ni mzuri na ana akili kiasi gani, kuna kitu kuhusu yeye kitakukatisha tamaa na kufanya mshindwe kwenda pamoja.
Dorian anamuomba Lord Henry pamoja na Basil waende naye kwenye nyumba ya sinema wajionee wenyewe.
Lord Henry anakubali, Dorian anamuomba pia amsaidie kumwambia Basil kwani hajaonana naye kwa muda mrefu na hataki kuwa naye peke yake. Anamwambia tangu amemjua Lord Henry ameona hawezi tena kukaa na Basil maana muda wote anaongea mambo ya maadili tu, wakati Lord Henry anaongea mambo mengi mazuri na ndiyo amempa ujasiri wa kuweza kupata mpenzi.
Lord Henry anamwambia hivyo ndivyo wasanii walivyo, wakifanya kazi bora za sanaa wanaweka kila kitu chao kwenye kazi hizo hivyo ukikutana nao unaona kama hawana maisha mengine. Lakini msanii akiwa anaeleweka kwenye maisha, basi kazi zake za sanaa siyo bora.
Dorian anaaga na kuondoka, Lord Henry anawaza jinsi amekuwa na ushawishi wa haraka kwa kijana huyo na kuona anaenda kasi sana, anakimbilia vitu ambavyo bado hajawa tayari navyo. Ila anajiambia kuna kikubwa cha kujifunza hapo na hivyo kuwa tayari kuona hilo linaendeleaje.
Baadaye anakuja kupokea barua kutoka kwa Doriana inayomfahamisha kwamba amemchumbia Sibyl Vane na muda si mrefu wataoana.

👉5
Sibyl anamwambia mama yake kwamba ana furaha sana amepata mchumba ambaye wanapendana sana.
Anamwambia yeye amempenda mchumba huyo kwa sababu ana muonekano mzuri na anaona anatoka familia tajiri. Ila hajui kwa nini mchumba huyo amempenda.
Anamwambia mama yake siku siyo nyingi wataoana na maisha yao ya shida ya kuigiza majukwaani kama malipo ya wale wanaowafadhili yatakuwa yameisha.
Mama yake anamuuliza jina la mwanaume huyo anaitwa nani, anamjibu hajajua jina lake hasa, ila huwa anamuita Prince Charming, kwa mwonekano wake mzuri.
Mama yake anamwambia awe na tahadhari, bado ni mdogo na hajajua mapenzi ni nini. Isitoshe hajamjua mwanaume huyo vizuri hivyo asiwe na mategemeo makubwa.
Sibyl anasisitiza wanapendana sana na mwanaume huyo na hakuna cha kuwatenganisha.
Wakiwa hapo mdogo wakr aitwaye James anakuja, anasafiri siku inayofuata kwenda Australia kutafuta maisha. Mama yake anamwambia aende akapambane ili aje kuiokoa familia.
James anamwambia mama yake amchunge sana Sibyl wakati yeye hayupo. Anamwambia amesikia kuna mwanaume yuko naye, ila ana wasiwasi naye ataishia kumuumiza. Anamsihi sana mama yake asimamie hilo kwa ukaribu. Mama anamwambia asiwe na wasiwasi.
James na Sibyl wanatoka kwenda matembezi ya mwisho kabla hajasafiri, wanafika kwenye bustani na kukaa kuwaangali watu wanaopita. Sibyl anamwambia jinsi fursa nyingi zilivyo mbele yake huko anakoenda. Anamwambia anamuacha na furaha kwa sababu amepata mwanaume wanayependana sana.
James anamwambia awe makini na huyo mwanaume, asije akaishia kumuumiza. Sibyl anamwambia hawezi kumuumiza, ni mwanaume mzuri sana hata yeye James akimuona mara moja atamkubali.
Wakiwa wamekaa hapo Dorian anapita kwa mbali, Sibyl anajaribu kumwonesha James lakini hamuoni.
James anamwambia japo anaondoka, iwapo mwanaume huyo atamuumiza kwa njia yoyote ile, akirudi atamtafuta mpaka ampate na amuue.
Sibyl anamtaka warudi nyumbani, hakupendezwa na kauli yake hiyo.
Nyumbani wakati anaagana na mama yake anarudia tena kumsisitiza, kwamba sasa amebaki na mtoto mmoja, amwangalie kwa karibu yasije kumtokea ambayo yalomtokea yeye mama yao, ambaye alilaghaiwa na mwanaume na kuzalishwa bila kuolewa.

Mama yake anamhakikishia Sibyl yuko kwenye mikono salama.
Sibyl ana miaka 17, huku James akiwa na miaka 16.

👉6
Lord Henry anakutana na Basil kwa chakula cha jioni na kumpa taarifa kwamba Dorian amechumbia na anataka kuoa.
Basil anashtushwa na taarifa hizo na kusema kwa Dorian anayemjua hilo haliwezi kutokea.
Lord Henry anamwambia mambo ndiyo yako hivyo, Basil anamuuliza kama atamruhusu Dorian kufanya hivyo.
Lord Henry anamjibu ameshachoka kuwapangia watu nini wanapaswa au hawapaswi kufanya kwenye maisha yao. Hivyo amemuacha Dorian huru, lakini pia anaona atafurahia kujifunza kupitia anachofanya.
Anaendelea kueleza kwamba anajua hata wakioana mapenzi waliyonayo sasa hayatadumu, baada ya miezi sita watakuwa wamechokana na hapo Dorian ataanza kukimbizana na mengine.
Lord Henry anasema atakuwa anafurahia kushuhudia hilo.
Basil anamwambia haamini kama anayosema ni kweli, alidhani anamjali sana Dorian kumbe siyo, Lord Henry anamjibu anamjali ndiyo maana anamwacha apitie hayo, asimzuie kupata raha ya muda mfupi.
Wakiwa hapo Dorian anafika, wanamuuliza nini kimetokea akachumbia na kupanga kuoana haraka hivyo.
Dorian anawaambia alikutana na Sibyl baada ya onesho na wakapigana mabusu, Sibyl akamwambia anajiona hana thamani ya kuwa mke wake na hapo Darian akamjibu yeye ndiyo kila kitu kwake.
Lord Henry anamwambia kwamba Sibyl alimwekea mtego na yeye amenasa, Dorian anajibu hajali, kwani anampenda sana.
Anaendelea kusema hajawahi kuwa na raha kwenye maisha yake kama sasa na katika raha hiyo hajali tena nadharia na falsafa za Lord Henry ambazo anasema hazina msingi mzuri.
Basil anamtaka awe makini asije kuharibu maisha yake kwa mtu asiye sahihi, Dorian anamjibu yuko makini.
Baada ya chakula anawataka wawahi kwenye ukumbi ili wakajionee wenyewe sifa za Sibyl ambazo amekuwa anawaambia, kwamba ni mrembo, ana akili na muigizaji mzuri sana.
Wanaondoka, Lord Henry na Dorian wanapanda gari ya Lord Henry huku Basil alichukia teksi. Kuanzia hapo Basil anahisi kilichokuwepo kati yake na Dorian kimevunjika, hakipo yeta. Anaona ukuta mkubwa umejengeka kati hao.

👉7
Wanafika kwenye ukumbi wa maonesho na kukaa kusubiria onesho la Romeo and Juliet ambalo Sibyl atacheza kama Juliet lianze.
Dorian anaendelea kumsifia Sibyl na kuwaambia Lord Henry na Basil kwamba wataenda kujionea kipaji alicho nacho, jinsi alivyo na uwezo wa kuibadili sanaa kuwa kitu cha kiroho na kuwaingia watu.
Lord Henry anajibu hakuna ambacho hajaona, ila yupo tayari kufurahia onesho.
Basil anamwambia Dorian asimsikilize Lord Henry, kama anayosema kuhusu Sibyl ni kweli basi ni mwanamke sahihi kwake na ndoa yao itakuwa bora. Anasema mwanzo hakuelewa ndiyo maana alipinga. Dorian anamshukuru kwa kumwelewa.
Onesho linaanza na Dorian anawataka wawe tayari kushuhudia. Mchezo wa kwanza unaanza, lakini Sibyl haonekani akicheza kwa ubora wake wa siku zote, habebi uhalisia aliokuwa anabeba siku za nyuma.
Watu wanavumilia na kuona labda mchezo wa pili atakuwa tofauti, nao unaanza na Sibyl hafanyi vizuri kabisa, watu wanaanza kuzomea na kutoka nje.
Mchezo wa pili unapoisha Lord Henry anawaambia ni bora waondoke, anasema ni kweli Sibyl ni mzuri na mrembo, ila kwenye uigizaji hakuna kitu, hana kipaji kabisa.
Dorian anakataa kwamba hataondoka, ataangalia mpaka mchezo wa tatu, anajibu akiwa na hasira kali.

Dorian anawaomba msamaha kwa muda waliopoteza na kuwataka waende na kumwacha, Basil anamwambia labda Sibyl ni mgonjwa kwa siku hiyo.
Lord Henry anamsisitiza Dorian waondoke na asibaki hapo, kwani Sibyl hana kipaji cha uigizaji, ila kwa mke anafaa. Anamwambia hata hivyo hataendelea kuigiza akishamuoa, hivyo asijali sana.
Dorian anawataka waondoke na wamuache.
Anaangalia onesho la tatu nalo linaisha, bado Sibyl amefanya vibaya.
Baada ya mchezo kuisha anaenda nyuma ya jukwaa kukutana na Sibyl, anamlaumu kwa nini amefanya vibaya hivyo, anamwambia amemdhalilisha sana mbele ya marafiki zake.
Sibyl anamwambia kabla hawajakutana, maisha yake yote alifikiria kitu kimoja tu, uigizaji na hivyo aliweza kuuvaa uhalisia kweli. Lakini tangu wamekutana na kubusiana, amekuwa akimfikiria yeye Dorian kwa muda mrefu. Na hapo uigizaji umekuwa siyo muhimu tena kwake, bali kilicho muhimu kwake ni yeye Dorian.
Dorian anamjibu hawezi kuendelea tena kuwa na yeye, alimpenda kwa sababu alijua ni mwigizaji mzuri, lakini sasa kwa kuwa hana tena kipaji cha uigizaji hana manufaa kwake.
Dorian anaendelea kumweleza kwamba alitegemea siku moja awe muigizaji mkubwa na maarufu na wapate sifa kubwa, ila hilo haliwezekani tena.
Sibyl anampigia magoti na kulia, anamuomba asimuache, anaahidi kujitahidi na kufanya vizuri zaidi kwenye uigizaji.
Dorian anakataa, anaondoka na kumwambia hatamtafuta tena.
Dorian anazunguka usiku kucha bila kujua yuko wapi, anapita sokoni na alfajiri anarudi nyumbani.
Anafika na kuiangalia picha yake aliyochorwa na Basil, anaiona ni tofauti na ilivyokuwa awali. Picha inaonesha sura ha ukatili tofauti na mwanzo.
Anajiuliza picha hiyo imebadilikaje? Anakumbuka siku ile anaiona picha kwa mara ya kwanza, alitamani picha ndiyo iwe inabadilika ila yeye abaki na uzuri wake.
Anajiambia huenda takwa lake limetimia, anaiangalia tena picha, kweli ina mabadiliko.
Anajiuliza je sura ya ukatili inayoonekana kwenye picha inatokana na nini. Anajiambia labda kwa kuwa amemuacha Sibyl.
Anaamua kwamba atarudi kwa Sibyl amuombe msamaha waendelee na mapenzi, atampenda alivyo na siyo kutaka awe namna fulani. Pia anajiambia hataenda tena kwa Lord Henry na hatakubaliana na ushawishi wake.
Anaamua kupumzika ili baadaye afanye hayo aliyopanga.

👉8
Dorian analala kupitiliza, anaamka saa sita mchana na mfanyakazi wake anamletea barua za siku hiyo. Anaona barua kutoka kwa Lord Henry anaiweka pembeni na kujiambia hataisoma kwa wakati huo. Anasoma barua nyingine, kuna zenye bili za kulipa na taarifa mbalimbali.
Anamwambia mfanyakazi wake anataka kupumzika hivyo yeyote akija kumuulizia amwambia hayupo.
Dorian anafunga mlango na kurudi tena kuiangalia picha yake, akiamini landa aliiona akiwa amechoka. Anaiangalia na bado iko vile ilivyobadilika, sura inaonesha ukatili fulani uliofanyika. Hilo linamfanya Dorian ahifie hatima ya maisha yake.
Anajiambia atarudi kwa Sibyl na kumuomba msamaha kisha atimize ahadi yao ya kuoana. Anaandika barua ya kumuomba msamaha Sibyl, anaeleza jinsi alivyochukua maamuzi yake kibinafsi na hatafanya tena hivyo. Anamuomba amsamehe na waendelee na mapenzi yao, atampenda alivyo na siyo kwa alichonacho.
Anamaliza kuandika barua anasikia mtu anagonga mlango kwa nguvu na kumtaka afungue, ni Lord Henry ambaye anasisitiza hataondoka mpaka afunguliwe.
Dorian anamfungulia, Lord Henry anaingia na kumpa pole kwa yaliyotokea. Dorian anamwambia ameshajifunza kwamba amefanya makosa na hivyo anataka kuyarekebisha.
Lord Henry anamuuliza anapanga kuyarekebishaje? Dorian anamjibu amepanga atarudiana na Sibyl na waoane. Lord Henry anamuuliza kwani hakusoma barua aliyomtumi asubuhi? Anajibu hakusoma. Anamwambia barua ilikuwa ni ya kumpa taarifa kwamba Sibly amejiua. Jaba baada ya onesho wakati

wanaondoka na mama yake, alisema kuna kitu amesahau na kurudi kwenye ukumbi, baadaye wanamkuta amekufa, wanahisi alikunywa sumu.
Dorian anaumizwa sana na taarifa hizo, anasema hilo ni kosa lake, yeye ndiye amepelekea Sibyl ajiue.
Lord Henry anamwambia ndiyo sababu yuko hapo, anataka amsaidie asije akajichanganya na lawama zikaja kwake, maana hiyo siyo njia nzuri kwa kijana kuyaanza maisha yake.
Dorian anasema hataweza kujisamehe kwa hilo, anatamani Sibyl angeweza kuwa hai amuombe msamaha.
Lord Henry anamwambia asiumie sana, hivyo ndivyo maisha yalivyo. Anamweleza kwamba anamuonea wivu, maana yeye pamoja na kuwahi kuwa na mahusiano mengi kwenye maisha yake, mwanamke hajawahi kujiua kwa ajili yake.
Lord Henry anamtaka asikae peke yake, jioni wawe na chakula pamoja na kwenda kwenye sinema.
Dorian anaona huo ni ukatili, lakini hana namna, anakubaliana na Lord Henry.
Baada ya Lord Henry kuondoka Dorian anaiangalia tena ile picha na kugundua ilibadilika na kuwa na sura ya ukatili wakati Sibyl amejiua. Anaona picha hiyo itakuwa inabeba madhambi yake yote, huku yeye akibaki hana hatia.
Bado haelewi hilo limewezekanaje, anatamani angeweza kuomba hilo likabadilika.
Lakini pia anajipa moyo kwamba hataupoteza uzuri wake milele na hivyo anachohitaji ni umakini ili asilete madhara kwa wengine.
Muda wa kwenda kukutana na Lord Henry unafika na anaondoka kwenda kwenye mkutano huo wa chakula cha jioni.

👉9
Basil anafika nyumbani kwa Dorian na kumwambia alimtafuta siku nzima ya jana na hakumpata.
Dorian anamjibu alienda kwenye sinema. Basil anashangaa, anamwuliza anawezaje kwenda kwenye sinema wakati mpenzi wake amekufa.
Dorian anamjibu hataki kusikia habari hizo tena, yaliyotokea yameshatokea na sasa anaangalia yajayo.
Basil anamwambia hakuamini kama ana roho ya aina hiyo, anamwambia kuna kitu kikubwa kimebadilika ndani yake, siyo yule Dorian aliyemjua.
Dorian anamjibu jana aliumizwa sana na kifo hicho, ila baada ya kukutana na Lord Henry ameweza kuvuka maumivu hayo na kuyaacha nyuma.
Basil anamuuliza kama ameshatafutwa kwenye upelelezi wa tukio hilo, Dorian anajibu hata jina lake hawalijui maana Sibyl alikuwa anamuita Prince Charming.
Dorian anamwambia Basil kama anataka urafiki wao uendelee basi aache kuongelea habari hizo.
Basili anakubaliana naye.
Basil anamwambia anataka aione picha aliyochora, Dorian anamjibu hawezi kuiona. Hilo linamshangaza Basil, iweje hawezi kuona picha aliyochora mwenyewe? Dorian anamwambia hawezi kuiona kamwe na kama atalazimisha kuiona basi kuanzia hapo hataongea naye tena maisha yake yote.
Basil anamwambia haitaki kwa ubaya, bali anataka kuiangalia kama inahitaji kuboreshwa zaidi kwani itapelekwa kwenye maonesho. Dorian anashangazwa zaidi, anamuuliza Basil nini kimemfanya abadilike, maana awali alikataa kwamba picha hiyo haitaenda kwenye maonesho.
Basil anamjibu mara ya kwanza anakutana naye alivutiwa naye sana na akageuka kuwa hamasa yake ya kisanaa, alitaka kuwa naye muda wote na hakutaka kumpoteza. Hivyo alipochora picha yake, aliweka kila kitu kilicho ndani yake na hapo hakutaka dunia iione. Lakini baada ya Dorian kuichukua picha, hali hiyo imeondoka na anajiona ni mjinga kutaka kuificha ndiyo maana amekubali ipelekwe kwenye maonesho.
Doriana anamwambia hataweza kuiona na pia haitaenda kwenye maonesho. Basil anamuomba basi aende tena studio kwake wachore picha nyingine, Dorian anamjibu hatafanya hivyo tena. Watakutana kama marafiki lakini siyo kwa ajili ya kumchora.
Basil anashindwa kuelewa nini kimetokea kwa Dorian ila anaamini ni ushawishi wa Lord Henry.

Anakubaliana naye na kuondoka.
Dorian anajiambia itabidi aifiche picha hiyo mbali sana, eneo ambalo hakuna yeyote anaweza kuiona kwa sababu hataki siri yake ijulikane.

👉10
Dorian anamwita mfanyakazi wake na kumtuma akamwitie watengeneza fremu za picha na kisha anampa barua ya kupeleka kwa Lord Henry ili asiwepo hapo na kushuhudia anakoficha picha.
Anamtaka mfanyakazi wa ndani ampe funguo za maktaba ya zamani, anamjibu ni chafu, haijasafishwa kwa miaka 5, labda isafishwe kwanza. Dorian anamwambia haina haja, ampe tu funguo kuna kitu anaangalia.
Watengeneza fremu wanakuja, anawaambia anataka wamsaidie kubeba picha na kuiweka kwenye chumba tofauti. Ameifunika picha kwa namna ambayo haionekani.
Wanaenda mpaka kwenye maktaba ya zamani, anaingia na kumbukumbu za utoto wake zinamjia, wakati babu yake akiwa hai na yeye kutumia muda wake mwingi kwenye maktaba hiyo.
Anawaelekeza pa kuiweka picha, wanataka kuiangalia ila anawakataza.
Wanaweka picha, anafunga mlango na kuweka funguo kwenye mfuko wake. Anajiambia sasa picha hiyo iko salama, aibu yake imefichwa.
Anarudi na kupokea ujumbe kutoka kwa Lord Henry ambapo amemtumia gazeti na kitabu. Gazeti linaelezea uchunguzi wa kifo cha Sibyl na kitabu ni riwaya inayomsisimua sana.
Muda wa kukutana na Lord Henry umepita, anaenda akiwa amechelewa na kumwambia kitabu alichomtumia ndiyo kimemchelewesha, wanaendelea na chakula cha jioni.

👉11
Kitabu ambacho Dorian amepewa na Lord Henry amekuwa anakisoma muda wote na hawezi kukiacha.
Anayaona maisha yake yakiwa kama maisha ya shujaa wa kitabu hicho, ambaye amejaribu kila starehe ya kila kizazi.
Kitabu hicho kinakuwa ndiyo mwongozo wa maisha yake na anachagua kuishi kama alivyoishi shujaa wa kitabu hicho, maisha ya kula raha muda wote.
Kunakuwa tetesi mbalimbali zinazosemwa kuhusu yeye, wengine wakisema ni mtu asiyejali na mwenye roho mbaya. Lakini watu wanapokutana naye, kwa uzuri wake na uso wa tabasamu, wanajikuta hawaamini tetesi zinazosemwa juu yake.
Vijana wengi wanatamani kuwa kama yeye, wanajaribu kuvaa na kuishi kama yeye.
Mara kwa mara amekuwa anaikumbuka picha yake na kwenda kuiangalia, anaona jinsi inavyozidi kubadilika kwa kuzeeka huku yeye akibaki vile alivyo.
Watu pia wanaanza kupata wasiwasi kuhusu Dorian, wanaoba dhahiri kwamba habadiliki.
Wanaomzunguka wanabadilika na kuzeeka ila yeye amebaki vile vile. Hilo linapelekea baadhi ya watu kuanza kumkwepa na kuepuka kukaa naye.
Amekuwa na hamasa ya kujifunza vitu kwa undani, kuna kipindi alijifunza kuhusu manukato na kuzama ndani kujua jinsi kila aina ya manukato inavyotengenezwa.
Akajifunza pia kuhusu miziki na kujua kila aina ya muziki mpaka wa makabila ya mbali na yenye siri kubwa.
Pia akajifunza kuhusu madini ya thamani, akajua namna watawala mbalimbali wa miaka ya nyuma walivyotumia madini kama alama ya madaraka na urembo pia.
Wasiwasi wake mkubwa bado upo kwenye picha yake, anahofia kuna siku watu wataigundua na hapo maisha yake yatakuwa wazi. Lakini anajipa moyo haya wakiiona picha, bado hawawezi kujua siri yake.
Kitabu ambacho Lord Henry alimpa kimekuwa sumu kubwa kwenye maisha yake, kwani kimemfanya awe na maisha ya tofauti sana.

👉12
Ni usiku wa kuamkia tarehe ya kuzaliwa kwake ambapo anatimiza miaka 38. Dorian anatoka nyumbani kwa Lord Henry usiku na kuelekea nyumbani kwake.

Njiani anakutana na Basil akiwa anatokea nyumbani kwake, anamwambia amemsubiri sana, anataka waongee kwani anasafiri kwenda Ufaransa na atakaa kwa muda mrefu.
Wanaingia ndani na Basil anamuuliza Dorian iwapo tetesi zinazosambaa kuhusu yeye ni za kweli.
Dorian anamjibu Uingereza imejaa tetesi za kila aina na hajisumbui nazo.
Basil anamweleza hapaswi kuzidharau tetesi hizo, kwani zinaharibu sifa yake. Anamweleza matukio mbalimbali ambayo amesikia, kwamba kila anayejihusisha naye anaharibikiwa au kujiua na baadhi ya watu wenye heshima wameanza kumkwepa Dorian.
Dorian anakasirishwa na hilo na kusema siyo kweli, watu wanayaharibu maisha yao wenyewe.
Basil anamwambia hamwelezi hayo kama kumkomoa, bali anataka kumsaidia aweze kuyaishi maisha yake vizuri na ajijengee sifa nzuri. Anamwambia kwamba ana ushawishi mkubwa kwa wengine, hivyo anapaswa kuutumia vizuri badala ya ilivyo sasa ambapo anasifika kwa anasa tu.
Basil anamweleza kinachomshangaza ni kwamba uso wake hauoneshi hatia. Anasema kwamba anajua mtu yeyote anayefanya jambo lisilo sahihi, hawezi kulificha, lazima uso wake au hata mikono itaonesha hatia. Lakini uso wa Dorian na hata mwili wake hauoneshi hatia yoyote.
Basil anamaliza kwa kumwambia anataka kusikia kutoka kwake kabla hajasafiri kwamba yote hayo siyo kweli. Anamwambia japo hawajawa karibu kwa muda, bado kwake ni rafiki anayemjali.
Anamwambia anatamani angeweza kuona roho yake na kujua kama kweli ni safi, ila hilo ni Mungu tu anaweza.
Dorian anamwambia leo atakwenda kuona roho yake na kupata majibu ya maswali yake yote.
Atajionea kwa macho yake nini kimekuwa kinaendelea.
Doriana anamtaka amfuate kwenye studio ya zamani, kuna kitu anataka kumuonesha, Basil anamfuata.

👉13
Dorian anaongozana na Basil mpaka kwenye chumba cha maktana ya zamani. Anafungua mlango na wanaingia, anaweka taa mezani na kumwambia sasa anaenda kuona roho yake, anamtaka afungue picha iliyo mbele yake.
Basil haelewi hilo linamaanisha nini, Dorian anaifungua picha ila na anachokiona Basil kinamshangaza. Ni mtu mwenye sura ya kutisha, sura yenye hatia na iliyozeeka. Anachoweza kutambua ni jina lake lililopo kwenye picha hiyo, hakumbuki kuwahi kuchora picha ya aina hiyo.
Dorian anamkumbusha siku alipokamilisha kuchora picha hiyo na maombi aliyosema, ndiyo yametimia.
Basil anakumbuka jinsi Dorian alivyoomba yeye abaki alivyo ila picha ndiyo ibadilike. Anamwambia Dorian kama huo ndiyo uhalisia basi hata yanayosemwa kuhusu yeye ni madogo kuliko yalivyo mazito kwenye uhalisia.
Basil anamtaka Dorian wapige magoti na kusali, waombe hali hiyo ibadilike. Dorian anamwambia wameshachelewa, hakuna kinachoweza kubadilika.
Basil anamkumbusha mistari ya biblia inayosema hata dhambi zenu zinapokuwa nyekundu kama damu, Mungu atazifanya nyeupe kama theluji, anamsisitiza sana wapige magoti na kuomba, kama maombi ya mwanzo yalivyosikika, ndivyo ya sasa pia yatasikika.
Hasira kali inamjia Dorian na kuchukua kisu kisha kumchoma Basil mpaka anakufa. Anatoka ndani ya chumba hicho na kukifunga.
Anafikiria namna ya kutatua hilo, anakumbuka Basil alimwambia anasafiri kwenda ufarasa, na usiku huo hakuna aliyejua kama bado yuko kwake. Hivyo akiweza kuficha hilo, kila mtu atajua Basil ameenda ufaransa, hakuna atakayehisi ameuawa.
Anaenda kwenye kitabu cha anwani na kuangalia anwani ya ‘Alan Campbell, anapanga kuonana naye asubuhi.

👉14
Dorian anaamka na kuandika barua mbili, moja anaweka mfukoni na nyingine anampa mfanyakazi wake apeleke kwa Alan Campbell.

Mawazo kuhusu kifo cha Basil yanamjia, anajaribu kuyaondoa lakini bado yanarudi.
Anajiambia kuruhusu mawazo hayo yamjie hakuwezi kumsaifia.
Anachukua kitabu na kukisoma ili abadili mawazo, lakini bado mawazo hayaondoki.
Anasubiri kwa shauku kubwa Alan Campbell aje, ndiyo tumaini lake kuu. Walikuwa marafiki zamani ila sasa siyo marafiki tena. Alan ni mwanasayansi ambaye ana maabara yake na amekuwa anafanya majaribio mbalimbali.
Kadiri muda unavyokwenda na haji anazidi kupata wasiwasi, vipi kama amesafiri, mwili huo hauwezi kukaa hapo muda mrefu.
Anasikia mtu anagonga mlango, anaingia ni mfanyakazi wake akiwa na Alan. Anamkaribisha Alan na kumruhusu mfanyakazi wake aende.
Dorian anamwambia Alan anashukuru kwa kuitikia wito wake, Alan anamjibu amekuja kwa sababu barua inaeleza ni jambo muhimu la maisha na kifo.
Dorian anamjibu ni kweli, kwenye chumba cha siri hapo kwenye nyumba yake, kuna maiti ya mtu ambaye hakuna anayejua kama iko hapo. Hivyo ni siri ambayo hakuna anayeijua, anachotaka kwake ni atumie uwezo wake wa kisayansi kuiteketeza maiti hiyo ili kusiwe na ushahidi kabisa.
Alan anamjibu hataweza kufanya hivyo, hataki tena kujihusisha naye na maovu yake. Anamtaka asiendelee kumweleza maana hatafanya chochote. Anamwahidi pia hatasema chochote.
Dorian anamsihi na kumwambia maiti hiyo isipoteketezwa itamletea shida, atapata kesi kubwa itakayopelekea ahukumiwe kifo, hayupo tayari kuharibu maisha yake.
Alan anamjibu hajali, hayupo tayari na yeye kuharibu maisha yake kwa kujihusisha na maovu yake.
Dorian anamwambia Alan kwa kuwa amekataa ombi lake, hana budi kutumia njia nyingine.
Anamwonesha barua nyingine aliyoandika, Alan anaisoma na ghafla anapatwa na hofu kubwa.
Dorian anamuuliza atamsaidia kwenye hilo au atekeleze mpango wake mwingine? Alan anamjibu atafanya lakini siyo kwa sababu anataka kumsaidia, bali kujiepusha mwenyewe na matatizo zaidi.
Alan anamtaka Dorian amruhusu akachukua vifaa kwenye maabara yake, Dorian anamjibu hapaswi kuondoka, aandike vitu anavyohitaji mfanyakazi wake akalete.
Alan anaandika, Dorian anampa mfanyakazi wake na anaenda kuvichukua.
Baada ya mfanyakazi kurudi anamtuma mbali na kumwambia asirudi mpaka jioni.
Anampeleka mpaka kwenye chumba ambacho mwili upo, Alan anaingia na kuanza kazi yake, anamtaka amuache peke yake.
Baada ya masaa matano Alan anatoka na kumwambia kazi aliyompa ameikamilisha na hataki kuongea naye tena maisha yake yote. Alan anaondoka.
Dorian anaenda kwenye kile chumba na kukuta mwili haupo, ila kuna harufu tu ya kemikali zilizotumika.

👉15
Jioni ya siku hiyo anahudhuria kwenye mwaliko wa chakula cha jioni. Anajiambia ameshasahau kila kitu kuhusu Basil.
Anafika kwenye chakula cha jioni na kukutana na watu mbalimbali Lord Henry akiwa mmoja wa waalikwa.
Wanaongea sana na wakati wa chakula Dorian anajikuta hana hamu ya kula chochote. Lord Henry anamuuliza leo ana shida gani? Dorian anajibu yuko sawa.
Wanaendelea na maongezi, aliyewaalika anasema Dorian anapaswa kuoa sasa na atamtafutia mwanamke atakayemfaa.
Lord Henry anatoa mawaidha yake kuhusu kuoa, akisema mwanaume anaweza kufurahia mwanamke yoyote ambaye hampendi. Akieleza wanawake wanaolewa ili kupata furaha, huku wanaume wakioa ili kupoteza furaha.
Aliyewaalika anamwambia Lord Henry kwamba falsafa zake ni za upotoshaji ndiyo maana watu wanamsema ni muovu. Lord Henry anamjibu hao ni wanafiki maana hawajawahi kumfuata na kumwambia hilo.
Dorian haonekani kujichanganya na wengine, Lord Henry anamuuliza jana walipoachana alifanya nini.

Anamwambia alienda klabu, akasema hapana, alizunguka mpaka saa nane ndiyo akarudi nyumbani, hata akimuuliza mfanyakazi wake atamwambia alirudi saa ngapi.
Lord Henry anashangazwa na jibu hilo la kujitetea, anamwambia Dorian anamjua vizuri, kuna kitu hakipo sawa. Dorian anamjibu anaomba waongee kesho, leo hajisikii vizuri.
Anarudi nyumbani na mawazo ya Basil bado yanamsonga, anachukua vitu vyake vilivyokuwa vimebaki na kuvichoma moto.
Anamuita dereva aje ampeleke sehemu ambayo ni ya mbali.

👉16
Dereva anampeleka mpaka nje kabisa ya mji, anashuka na kuelekea kwenye nyumba iliyojificha. Ni nyumba inayouza vilevi mbalimbali haramu.
Dorian anaona hiyo ndiyo njia pekee ya kufuta kumbukumbu za Basil, kwa kutumia madawa ya kulevya.
Anafika pale na kukuta watu wengi wakiwa wanatumia vilevi vyao, mwanamke anayemfahamu anaanza kumzongazonga, anampa fedha ili amuache.
Anaingia vyumba vya ndani na kukutana na mtu mwingine wanayefahamiana, anashangaa kumbe bado yupo maana alisikia ameondoka.
Anaongea naye kwa muda na kuamua hapo kuna wengi wanamjua, hivyo ataenda kwenye nyumba nyingine.
Wakati anatoka yule mwanamke anamuona, anasema muovu huyo anaondoka, Dorian anamtaka aache kumwita hivyo.
Mwanamke yule anacheka na kumuuliza anataka amuiteje? Amuite Prince Charming?
Dorian hajibu, anaondoka ghafla anasikia mtu anamkimbilia na kumkaba roba. Anamshikia bastola na kumwambia leo siku yake imefika.
Dorian anamuuliza amemkosea nini? Mtu huyo anamjobu amekuwa anamtafuta mwanaume aliyesababisha dada yake ajiue, alikuwa hajui jina lake, ila leo aliposikia Prince Charming akajua ndiye yeye, maana ndivyo dada yake alimuita.
Anamkumbusha dada yake ni Sibyl na yeye ni James, alijiapiza atamuua atakayemdhuru dada yake.
Anampa Dorian dakika moja ya kutubu maana atamuua. Dorian anapata akili ya haraka. Anamuuliza dada yako alijiua lini? James anamjibu miaka 18 iliyopita. Dorian anamtaka wasogee kwenye mwanga na aone sura yake.
Wanaenda kwenye mwanga, James anashangaa ni sura ya kijana wa miaka 20, anamuomba msamaha kwa kumdhania vibaya, mtu anayemtafuta atakuwa anakaribia miaka 40.
Dorian anamtaka awe makini na asitafute kulipa kisasi, kwani atadhuru wasio sahihi, anaondoka na kumwacha.
Yule mwanamke anatoka na kumkuta James akiwa amesimama pale kwa mawazo, anamuuliza kwa nini hajamuua? James anajibu siyo mtu aliyekuwa anamtafuta, anayemtafuta ni mtu ambaye umri wake ni mkubwa.
Mwanamke yule anamwambia asidanyanyike na sura, Dorian ni mkubwa, kwani yeye amemjua miaka 18 iliyopita na yuko hivyo hivyo habadiliki.
James anamuuliza kama anayosema ni kweli, mwanamke yule anamjibu ni kweli kabisa.
James anatoka haraka kumkimbilia Dorian lakini hamuoni tena.

👉17
Dorian amehamia kwenye nyumba yake iliyo nje ya mji ili kuepuka hatari ya kukutana tena na James.
Wiki moja baadaye Dorian ameandaa chakula cha jioni na kuwaalika watu mbalimbali. Lord Henry ni mmoja wao.
Wanakuwa na mazungumzo mbalimbali na kama kawaida Lord Henry anatoa falsafa zake za maisha ambazo zinawashangaza wengi.
Safari hii anawaambia siri ya maisha ni mtu kurudia tukio kubwa ambalo amewahi kupitia kwenye maisha. Wanamuuliza hata kama ni la kuumiza, anajibu ndiyo.

Mgeni mmoja anamuuliza Dorian kama anakubaliana na Lord Henry kwenye hilo, anajibu anakubaliana na kila anachosema. Anamuuliza hata anapokosea, anajibu huwa hakosei. Anamuuliza tena je kufuata falsafa zake kunampa furaha, anajibu hatafuti furaha bali raha, ambayo huwa anaipata mara kwa mara.
Dorian anawaacha wamekaa na kuingia ndani, wanasikia sauti ya mtu analia, kwenda wanakuta Dorian amedondoka na kuzimia. Anapostuka anauliza nini kimetokea, Lord Henry anamjibu amezimia, inaonekana amechoka sana, anamtaka apumzike.
Akiwa chumbani kwake Dorian anaangalia nje kupitia dirishani na kuiona sura ya James kwa mbali, hilo linampa hofu zaidi.

👉18
Siku inayofuata hatoki chumbani kwake, kila akifumba macho anaiona sura ya James, anajiambia ni fikra zake zinampa hofu, kwani hawezi kufika hapo.
Pamoja na kujiambia hivyo bado hapati utulivu, anaona maisha yake yako kwenye hatari kubwa.
Siku inayofuata anatoka na kuungana na wageni wake, siku hiyo baadhi wanawinda kwenye pori lililo pembeni ya nyumba hiyo.
Mmoja anamuona sungura akipita na kulenga bunduki yake ili amuue, Dorian anamkataza asimuue sungura huyo, amuache aishi.
Mtu huyo anamcheka, anamwambia kwa nini aonee sungura huruma kama mwanadamu, anafyatua risasi na inasikika milio miwili, wa sungura na wa mtu aliyeumizwa.
Wasaidizi wanaenda kwenye pori hilo na kukuta kuna mtu alikuwa hapo amepigwa risasi. Dorian anawaambia kwa nini wanakosa umakini mpaka watu wanapita kwenye hilo eneo la mawindo.
Mtu huyo amekufa na kwa kuwa amepigwa risasi kwa bahati mbaya, Dorian anawataka wasaidizi wake wafuatilie kuhusu familia yake ili waweze kuisaidia.
Wanaahirisha zoezi la uwindaji na kurudi ndani. Dorian anamwambia Lord Henry itabidi aondoke, anaona sehemu hiyo siyo salama kwake, tukio lililotokea ni ishara mbaya, huenda kitu kibaya zaidi kikatokea.
Lord Henry anamwambia anajipa hofu tu.
Dorian anaenda chumbani kwake, anamtuma msaidizi wake akaandae usafiri wa yeye kuondoka siku inayofuata kisha anaandika barua kwa ajili ya Lord Henry akimweleza anaondoka kwenda kumwona daktari kwa kuwa bado hajisikii vizuri, yeye abaki na wageni mpaka atakaporudi.
Akiwa hapo mfanyakazi anayetunza pori wanalowinda anakuja na kumwambia mtu aliyekufa hajulikani, ni mtu mgeni maeneo hayo ila anaoneoakana kama ni baharia.
Dorian anashtushwa na taarifa hizo, anasema apelekwe akamuone. Anafika na wanafunua uso wake, anagundua ni James.
Dorian anaondoka huku akijiambia kwa sasa yuko salama.

👉19
Dorian bado yuko nje ya mji, Lord Henry amemtembelea na anamweleza msichana aliyekutana naye anaitwa Hetty.
Dorian anasema japo si wa daraja lake, lakini amempenda kweli na anaahidi kubadilika ili aweze kumuoa.
Lord Henry anamwambia jinsi alivyo amekamilika, hahitaji kubadili chochote. Anamwambia maisha yake ameishi kwa raha wakati wote, hana hatia yoyote. Dorian anamjibu asiseme hivyo kwa kuwa hamjui kwa ndani.
Dorian anamuuliza ni habari gani zinaendelea huko mjini, Lord Henry anamjibu bado watu wanazungumzia kupotea kwa Basil, maana Ufaransa hajaonekana. Dorian anauliza watu hawana vitu vingine vya kufuatilia mpaka wafuatilie hilo muda wote?
Lord Henry anamjibu pia kuna habari nyingine mpya, Alan Campbell amejiua, mke wake amempa talaka na kuna msanii mwingine amepotea pia haonekani.
Dorian anamuuliza kama watu wanasema Basil ameuawa, anajibu hakuna mwenye uhakika.

Anamuuliza yeye hafikirii kama Basil aliuawa, anajibu pamoja na kuwa msanii mkubwa, Basil hakuwa na kitu cha kumfanya awe na maadui, hivyo hadhani ameuawa, labda amejificha tu kama ilivyo kawaida yake au alikufa kwa ajali na hakuna aliyejua.
Dorian anamwuliza vipi kama akimwambia yeye ndiye amemuua Basil, Lord Henry anacheka sana na kumwambia hiyo ni dhambi ambayo hana ujasiri wa kuifanya, maisha yake ni makamilifu sana kufanya kitu cha aina hiyo.
Dorian anaenda kwenye kinanda na kuanza kupiga, Lord Henry anamwambia aendelee kupiga kwani inamfanya ajisikie vizuri. Anamuomba Dorian ampe siri yake ya kubaki kijana, kwani mwonekano wake haujanadilika tangu wamejuana, wakati yeye amezeeka na nguvu zimepungua.
Anamwambia na sasa ana upweke baada ya mke wake kumuacha, japo anaamini ndoa siyo kitu bora, lakini ukishazoea kitu ukikikosa unaumia.
Anamsifia Dorian kwamba amekuwa na maisha ya raha, hajawahi kusumbuka kwa chochote, kama ni siri ya maisha basi yeye anaijua.
Dorian anamwambia asiseme hivyo, kuna mengi ambayo hayajui kuhusu yeye, kama akiyajua hatataka kuwa rafiki yake tena.
Lord Henry anamwambia wakutane siku inayofuata mchana kuna mtu atakwenda kumkutanisha naye.

👉20
Dorian anapita njiani, vijana wawili wanampita na anawasikia wakiambiana huyo ni Dorian Gray, ameshachoka kusikia kina lake.
Mpango wake sasa ni kuanza maisha mapya na mpenzi wake Hetty ambaye hajui mengi kuhusu yeye.
Anafika nyumbani na kukaa kwenye kiti, anakumbuka mazungumzo yake na Lord Henry ambaye alimwambia hawezi kubadilika, anajiuliza kama hilo ni kweli.
Anayatafakari maisha yake na kuona sasa ana nafasi ya kuanza upya, James ameshakufa hivyo hakuna anayemuwinda. Alan amejiua bila kutoa siri hivyo hakuna anayejua kuhusu kifo cha Basil. Na kwa kifo cha Basil, hakuna ushahidi wowote unaomhusisha yeye.
Anajisikia vizuri kwamba sasa ana fursa ya kuanza maisha yake upya, kuwa mtu mwema na kutokufanya tena uovu wowote.
Anajiambia kwa mabadiliko hayo huenda picha yake nayo ikawa imeanza kubadilika.
Anachukua taa na kwenda kwenye chumba ilipo picha, anaiangalia na kukuta imezidi kuwa na sura ya ukatili.
Anajiuliza afanye nini sasa, je picha hiyo inamtaka akiri makosa yake? Na hata akikiri, nani atakuamini na hakuna ushahidi?
Anajiambia kwa kuwa ameshamuua mchoraji wa picha na anataka kuanza maisha upya, lazima aharibu picha hiyo.
Anachukua kisu alichomuua nacho Basil na kuichoma picha ile kwa kisu hicho, inasikika sauti kubwa ya maumivu.
Wafanyakazi wake wanatoka kuangalia nini kinaendelea, wanagonga mlango wa chumba hicho haufunguki.
Wanavunja na kuingia, wanakuta picha ya Dorian ikiwa na sura nzuri na ya ujana kama ambavyo amekuwa anaonekana. Hapo chini pakiwa na mtu ambaye sura yake ni ya kikatili na umri wake unaonekana kuwa mkubwa, akiwa amechomwa kisu kifuani.
Wanakagua mwili wa mtu huyo na kuukuta ukiwa na pete ya Dorian, hapo ndipo wanajua kwamba ule ni mwili wa Dorian Gray.

👉Tunayojifunza.
Riwaya hii ambayo imeandikwa zaidi ya miaka 100 uliyopita, ina mengi ya kutufundisha kuhusu maisha. Imebeba mafunzo na falsafa nyingi za maisha ambazo tukijifunza tutaweza kuwa na maisha bora.
1. Tunajifunza jinsi ushawishi wa wengine unaweza kuwa na nguvu kwetu na kupelekea kuyaharibu kabisa maisha yetu. Kwa hili tunapaswa kuwa makini na wale tunaowasikiliza, hasa wanaotuambia

yale tunayopenda kusikia.
2. Tunajifunza siyo yote tunayotamani yana manufaa kwetu. Kuna vitu unatamani sana uwe navyo, lakini ukivipata vinaishia kuwa mateso kwako kwa maisha yako yote.
3. Tumeona jinsi ambavyo mtu hawezi kufanya uhalifu mmoja na akaishia hapo, hasa anapouficha. Ukifanya uhalifu na kuuficha, utakusukuma kufanya uhalifu mwingine ili uendelee kutunza siri unayoficha.
4. Tumejifunza kuwa makini na hisia zetu na za wengine pia. Ni rahisi sana kuvunja hisia za wengine kwa kujali hisia zetu pekee, kitu kinachoweza kuleta madhara makubwa kwa wengine.
5. Huwa tunapata marafiki wazuri na wabaya kwenye maisha, lakini ni rahisi kuona marafiki wazuri wanachosha na marafiki wabaya ndiyo wanatuhamasisha, tunawaamini hao wabaya na wanaishia kutuharibu.
6. Maisha siyo kutafuta raha tu muda wote, maisha ya aina hiyo huwa na utupu mkubwa mwishoni na mtu huoni umeyaishije maisha yako. Tunapaswa kulijua kusudi la maisha na kuliishi ili kuwa na maisha ya furaha inayodumu badala ya kukimbizana na raha zisizodumu.
7. Kama unampenda mtu, mpende kama alivyo na siyo kumpenda kwa kile alichonacho, kila mtu hupoteza alichonacho, ila yeye anabaki, ukimpenda alivyo hutakatishwa tamaa.
8. Watu unavyowaona kwa nje sivyo walivyo kwa ndani. Kila mtu ana siri zake za ndani ambazo ukizijua hutataka hata kumkaribia. Hivyo usijilinganishe maisha yako na wengine kwa yale unayoona nje, kila mtu anapambana na vita fulani kwenye maisha yake.
9. Unaweza kutamani maisha ya mwingine, kumbe na yeye anatamani maisha yako. Kila aina ya maisha yana gharama ambayo mtu analipa. Ukiwa tajiri kuna gharama za kimaisha unalipa, kadhalika uliwa masikini. Ukiwa na mwonekano mzuri kuna gharama utalipa kadhalika ukiwa na mwonekano mbaya. Kwa kifupi hakuna kinachokuja bure kwenye maisha yako.
10. Uovu huwa haufichiki hata ufanye nini. Unapofanya uovu wowote, kuna vitu vingi vinabadilika ndani yako na wale wanaokujua wanajua vizuri kwamba haupo sawa. Hivyo kazana kutokutenda uovu kwenye maisha na pale unapokuwa umeutenda basi usiufiche, badala yake ukiri ili uweze kuwa na maisha huru. Hata kama unaona ukikiri uovu itapelekea upate kifo, kuuficha ni kuchagua maisha ya mateso yatakayoishia na kifo.

Muhtasari huu umeandaliwa na Kocha Dr Makirita Amani,
www.t.me/somavitabutanzania